

Kufanya kazi Australia

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako

Wakati unapofanya kazi hapa Australia na umeajiriwa, wewe utapata kulipwa mshahara na lazima ulipe ushuru kwa mshahara unaopata.

Kulipwa kwa ajili ya kazi

Wakati unapolipwa unapewa karatasi inayoonyesha mshahara. Kijikaratasi cha mshahara huonyesha kiasi cha pesa ulicholipwa, kiasi cha ushuru ulicholipa na kiasi cha pesa za uzeeni kilichowekwa kwenye akaunti ya uzeeni.

Ushuru

Wakati unapofanya kazi hapa Australia wewe utalipa ushuru kwa Serikali ya Australia ili serikali ipate pesa za kutolea huduma kwa mahitaji ya jumuiya, kama hospitali, shule, barabara na usafiri wa umma (basi na gari la moshi).

Nambari ya faili ya ushuru

Kila mtu hapa Australia anayo nambari yake ya kipekee ya faili ya ushuru (Tax File Number). Wewe unahitaji nambari ya faili ya ushuru ili kufanya kazi hapa Australia. Wakati unapoanza kazi, ni lazima wewe utoe nambari yako ya faili ya ushuru kwa mwaajiri wako.

Pesa za uzeeni

Hii ni pesa ambayo inawekwa akiba kwa ajili ya wakati unapozeeka na hufanyi kazi tena. Inawekwa kwenye akaunti ya pesa za uzeeni na mwaajiri wako.

Kumbuka

- ▶ Wakati unapofanya kazi hapa Australia na umeajiriwa, wewe utalipwa mshahara.
- ▶ Wakati unapofanya kazi hapa Australia, wewe unalipa ushuru (pesa) kwa Serikali ya Australia.
- ▶ Pesa za uzeeni ni pesa zinazowekwa akiba kwa ajili ya wakati ukiwa mzee na hufanyi kazi tena.
- ▶ Mwaajiri wako kwa kawaida lazima alipe kiasi zaidi cha asilimia tisa (9%) ya pesa unazopata kwa mshahara kwenye pesa za uzeeni kwa ajili yako. Pesa hizi ni kiasi zaidi ya mshahara wako.

Mahali pa kupata usaidizi na maelezo zaidi

Kwa maelezo zaidi ya pesa za uzeeni, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au piga simu 1300 300 630.

Kama unapata shida na mwaajiri wako au unataka kujua zaidi haki zako kama mfanyakazi, wasiliana na tuvuti ya Fair Work Australia, www.fwa.gov.au, au piga simu 1300 799 675.



Michael anaanza kazi yake mpya

Michael amekuwa hana kazi na kwa miezi tatu na amekuwa akipata malipo ya Centrelink ili kumsaidia yeye kununua vitu anavyohitaji.

Aliona tangazo la kazi ya muuzaji katika duka la nguo la mtaa. Alitia ombi, akaenda kwenye mahojiano na akaipata ile kazi.

Michael basi alipata barua iliyokuwa na maelezo zaidi kuhusu kazi mpya kutoka mwaajiri wake mpya.

Michael aliisoma ile barua. Ilisema kuwa jina la mwaajiri wake ni Jack Smith na kampuni inaitwa Clothes for Us. Pia barua ilisema kuwa kazi inaitwa 'muuzaji nguo', kuwa Michael atalipwa \$16 kila saa na atakuwa akifanya kazi kwa muda kwa masaa 25 kila wiki.

Baada ya kufanya kazi kwa wiki 2, Michael alipokea mshahara wake wa kwanza. Pia alipata kijikaratasi cha mshahara. Yeye angeweza kuona kiasi cha pesa alizolipwa, ushuru aliyolipa na kiasi cha pesa za uzeeni ambacho mwaajiri wake alilipa kwenye akaunti yake ya uzeeni.

Kwenye kijikaratasi cha malipo, Michael aliona kuwa alipata mashahara \$800 kwa kufanya kazi kwa wiki 2 na kuwa alilipwa \$85 kwenye ushuru. Pia aliona kuwa mwaajiri wake alilipa \$72 kwenye akaunti yake ya pesa za uzeeni.

Wiki iliyofuata, Michael alipokea malipo kutoka Centrelink.

Michael alijuwa kuwa ni muhimu kuwaambia Centrelink kuhusu kazi yake mpya ili waweze kufanya mabadiliko kwa kiasi wanachomlipa. Kutowaambia Centrelink inamaanisha kuwa Michael angeweza kulipwa pesa nyingi zaidi na Centrelink na basi atajipata kuwa na deni. Itambidi kuwalipa deni au ajipate kwenye shida.

Michael aliwapigia simu Centrelink kuwaambia kuhusu kazi yake mpya na akawatumia nakala ya barua kutoka mwaajiri wake.

This page has been intentionally left blank.